# GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

**18 AGOSTI 2026**

***Hupigwa Chapa kwa Idhini ya Serikali na Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti*** ***Hutolewa kila Ijumaa***

***Bei Tshs . 5000/=*** **CXXXV Nam. 7530**


**YALIYOMO** *Ukurasa*


Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali na kuweka masharti bora ndani yake: ....................................................................1103


## SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Mswada lililotajwa hapo chini linatangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

### Tangazo la Mswada

**Nam:** Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali na kuweka masharti bora ndani yake:

### TANGAZO

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanza tarehe 9 Septemba, 2026 kwa kusomwa kwa mara ya kwanza na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

**ZANZIBAR**
18 Agosti, 2026

(Ndugu Mansura Mosi Kassim)
***Katibu wa Baraza la Mapinduzi***
***na Katibu Mkuu Kiongozi.***


**Matangazo yaliyohusu Waliofariki na Mali wa Watu waliofariki, kuvunja Mikataba ya ushirikiano, taarifa za Makampuni, Upotevu na marekebisho ya Nyaraka za Serikali na mengineyo ambayo ni muhimu kwa Umma lazima kuchapishwa katika Gazeti Rasmi. Nakala za Matangazo hayo zipelekwe kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania SLP 261 Maruhubi, Zanzibar. Nakala ziwasilishwe kabla ya Siku ya Alhanisi ya kila Wiki**

# MSWADA
# wa
# SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, 2026 na itaanza kutumika mara tu baada ya kutiwa saini na Rais.

Marekebisho ya Sheria mbalimbali.

**2.** Sheria zilizotajwa katika sehemu mbalimbali za Sheria hii zinarekebishwa kwa namna zilivyoainishwa katika sehemu husika.

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UDHIBITI WA UTAKATISHAJI WA FEDHA HARAMU NA MAPATO YATOKANAYO NA UHALIFU, NAM. 10 YA 2009

Kusomwa.

**3.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Udhibiti wa Utakatishaji wa Fedha Haramu na Mapato Yatokanayo na Uhalifu, Nam. 10 ya 2009 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 10.

**4.** Kifungu cha 10 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta maneno "na kutumia njia sahihi za kudhibiti viashiria hatarishi" yaliopo mwisho wa kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake maneno "kutokana na taarifa ya tathmini na ufahamu wa viashiria hatarishi, mbinu za kutathimini viashiria hatarishi zitatumika katika kuweka rasilimali za kutosha na kuelekeza hatua ipasavyo ili kuzuia au kupunguza viashiria hatarishi vilivyobainishwa"; na

(b) kufuta maneno "ya mwaka" yaliyopo mwisho wa kifungu kidogo cha (11) na kuweka badala yake maneno "katika kila miaka mitatu."

Marekebisho ya kifungu cha 10C.

**5.** Kifungu cha 10C cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake kifungu kidogo cha (2) kipya kama ifuatavyo:

"(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, endapo mteja ni:

(a) mtu mwenye wadhifa maalumu kutoka nchi ya kigeni, mtoa taarifa:

(i) ataweka mifumo ya kusimamia viashiria hatarishi ili kutambua kama mteja au mmiliki mnufaika ni mtu mwenye wadhifa maalumu;

(ii) atapata idhini ya uongozi wa juu kabla ya kuanzisha uhusiano wowote wa kibiashara au kuendeleza uhusiano wa kibiashara na mteja huyo;

(iii) atachukua hatua stahiki kubaini chanzo cha mali na fedha za mteja na mmliki mnufaika aliyetambuliwa kama mtu mwenye wadhifa maalumu; na

(iv) atafanya ufuatiliaji endelevu juu ya uhusiano ulioelezwa katika kipengele cha (ii) cha aya hii;

(b) mtu mwenye wadhifa maalumu wa ndani ya nchi, mtoa taarifa:

(i) atachukua hatua stahiki kutambua kama mteja au mmiliki mnufaika ni mtu aliyetambuliwa chini ya kifungu hiki; na

(ii) endapo kutakuwa na viashiria vikubwa hatarishi vya mahusiano ya kibiashara na mtu huyo, atatumia hatua zilizoainishwa katika kifungu kidogo cha (2)(a)(ii), (iii) na (iv) cha kifungu hiki."

**SEHEMU YA TATU**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA MWENENDO WA JINAI, NAM. 7 YA 2018**

**6.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mwenendo wa Jinai, Nam. 7 ya 2018 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama". Kusomwa.

**7.** Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa: Marekebisho ya kifungu cha 2.

(a) kufuta ufafanuzi wa maneno "lalamiko" na "mlalamikaji" na kuweka badala yake ufafanuzi wa maneno mapya kama ifuatavyo:

"lalamiko" maana yake ni tuhuma zilizofanywa kwa njia ya maandishi mbele ya mahakama kwa lengo la kuchukua hatua ya kisheria chini ya Sheria hii;

"mlalamikaji" katika mashtaka binafsi maana yake ni Mwendesha Mashtaka Binafsi na katika mashtaka ya umma maana yake ni Mkurugenzi wa Mashtaka anayewasilisha kesi mbele ya mahakama kwa niaba ya Serikali;"

(b) kuongeza ufafanuzi wa maneno katika mpangilio wake wa kialfabeti kama ifuatavyo:

"mtegemezi" maana yake ni mzazi, mwenza au mtoto wa muhanga;

"muhanga" maana yake ni:

(a) mtu ambaye kosa limetendwa dhidi yake;

(b) mtegemezi wake au ndugu wa karibu ambaye kosa limetendwa dhidi yake ikiwa mtu huyo amefariki; au

(c) mtu ambaye sheria au mazingira yatakavyohitaji.

Kuongeza vifungu vipya vya 42A na 42B.

**8.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza vifungu vipya vya 42A na 42B mara baada ya kifungu cha 42 kama ifuatavyo:

"Taarifa inayohusiana na kutendeka kwa kosa.

**42A.-**(1) Taarifa inayohusiana na kutendeka kwa kosa kwa mujibu wa kifungu cha 370 cha Sheria hii inaweza kutolewa kwa mdomo au maandishi.

(2) Taarifa yoyote chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki itarikodiwa katika namna kama ilivyoelezwa chini ya masharti ya kifungu cha 42B cha Sheria hii.

(3) Afisa upelelezi yeyote anaweza, kwa maandishi, kumtaka mtu yeyote kufika mbele yake, ambaye, kutokana na taarifa zilizotolewa au katika njia nyengine yoyote inaonekana anajua mazingira au matukio ya kesi, au mtu ambaye anamiliki waraka au kitu chengine kinachohusiana na upelelezi wa kesi kuhudhuria au kutoa maelezo, waraka huo au kitu chengine chochote, na mtu huyo atahudhuria na kutoa maelezo hayo au nakala ya waraka huo iliyothibitishwa au kitu chengine kama itakavyohitajika.

(4) Endapo afisa upelelezi amepokea nakala ya waraka iliyothibitishwa au kitu chengine chochote, atatoa risiti kwa mtu ambaye ametoa waraka au kitu hicho.

(5) Taarifa yoyote iliyotolewa na mtu yeyote chini ya kifungu hiki inaweza kutumika kama ushahidi kwa mujibu wa masharti ya sheria inayotumika wakati huo kuhusiana na kosa linalohusika.

Upelelezi unaofanywa na afisa upelelezi.

**42B.-**(1) Afisa upelelezi yeyote anaweza kumhoji kwa mdomo mtu yeyote anayeaminika kujua matukio na mazingira ya kesi na ataweka kwa maandishi maelezo yatakayotolewa na mtu huyo anayehojiwa.

(2) Afisa upelelezi, kabla ya kumhoji mtu, atamueleza mtu huyo kuwa anawajibu wa kujibu maswali

yote yanayohusiana na kesi kwa usahihi na kwamba hawezi kukataa kujibu swali lolote kwa sababu tu swali hilo linaelekea kumuhusisha na kosa la jinai, adhabu au utaifishaji wa mali yake.

(3) Maelezo yote, ikijumuisha swali lolote la ufafanuzi lililoulizwa na afisa upelelezi na jibu lake, yatarikodiwa kwa ukamilifu kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza, na rikodi hiyo itaoneshwa au kusomwa mbele ya mtu huyo, na kama haelewi lugha ambayo maelezo yamerikodiwa, yatatafsiriwa katika lugha anayoifahamu na atakuwa huru kueleza au kuongeza kitu kwenye maelezo yake.

(4) Mtu aliyehojiwa atasaini maelezo aliyoyatoa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, chini ya mstari wa mwisho wa maelezo hayo yaliyorikodiwa, na anaweza kumuita mtu yeyote aliyekuwepo kusaini kama shahidi.

(5) Afisa upelelezi anayerikodi maelezo ataambatanisha chini ya kila maelezo aliyoyarikodi uthibitisho kwamba alirikodi kwa uaminifu na usahihi maelezo ya mtu aliyechunguzwa.

(6) Maelezo yanayotolewa na mtu yeyote kwa afisa upelelezi wakati wa upelelezi wowote, yanaweza kutumiwa kwa mujibu wa masharti ya sheria inayotumika wakati huo inayohusiana na utaratibu wa utoaji na upokeaji wa ushahidi.

(7) Katika shauri lolote chini ya Sheria hii, utoaji wa nakala iliyothibitishwa ya taarifa iliyotajwa chini ya kifungu cha 42A cha Sheria hii au maelezo yoyote yaliyowekwa katika kumbukumbu chini ya kifungu hiki, yatakuwa ni uthibitisho wa awali wa maelezo kuwa taarifa iliyotolewa au kwamba maelezo hayo yaliyotolewa kwa afisa upelelezi aliyerikodi na bila ya kujali masharti ya sheria nyengine yoyote, haitakuwa lazima kumuita afisa upelelezi kama shahidi kwa madhumuni ya kuwasilisha nakala iliyothibitishwa.

(8) Mtu yeyote ambaye ameitwa kuhudhuria au kutoa waraka au kitu chengine chochote kinachohusiana na upelelezi wa kesi chini ya masharti ya kifungu 42A cha Sheria hii au kifungu hiki, anakataa au kwa makusudi anapuuza kufanya hivyo, au ni shahidi kwenye upelelezi husika, anakataa kujibu swali lolote analoulizwa au kutoa waraka wowote au kitu chengine chochote kinachohusiana na upelelezi, ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyozidi Shilingi Laki Tano au kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja au vyote kwa pamoja.

(9) Pamoja na adhabu iliyoainishwa chini ya kifungu kidogo cha (8) cha kifungu hiki, mahakama inaweza kumuamuru mshtakiwa kufanya kile ambacho alitakiwa kukifanya na afisa mpelelezi."

Kuongeza kifungu kipya cha 79A.

**9.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 79A mara baada ya kifungu cha 79 kama ifuatavyo:

"Usafirishaji uliodhibitiwa, mtego na operesheni ya siri.

**79A.-**(1) Afisa upelelezi anaweza kutumia mbinu ya usafirishaji, mtego au operesheni ya siri iliyodhibitiwa ili kutambua, kupeleleza au kufichua uhalifu na ushahidi uliopatikana utakubaliwa na mahakama ikizingatiwa kwamba:

(a) kabla ya kuweka mbinu ya usafirishaji, mtego au operesheni ya siri iliyodhibitiwa, ruhusa iliyohitajika ilitolewa na mkuu wa kituo cha polisi, mkuu wa taasisi ya upelelezi au afisa yeyote aliyeidhinishwa na yeye kutumia mbinu hizo za upelelezi na kwa mujibu wa maelekezo yaliyotolewa;

(b) kuwepo kwa mbinu nyengine kwa ajili ya utambuzi, upelelezi, kufichua kufanyika kwa kosa au kuzuia kosa lisitokee katika mazingira maalumu na katika sehemu husika;

(c) ikiwa kabla ya kutumia mbinu ya usafirishaji, mtego au operesheni ya siri iliyodhibitiwa, kuna shaka yoyote na sababu za msingi kwamba mtuhumiwa amehusika na kosa; au

(d) ikiwa afisa amefanya kwa nia njema.

(2) Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kutoa miongozo ya jumla au maalumu kuhusu usimamizi na udhibiti wa mbinu za usafirishaji, mitego na operesheni za siri."

Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 104, 105 na 106.

**10.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kufuta vifungu vya 104, 105 na 106 na kuweka badala yake vifungu vipya vya 104, 105 na 106 kama ifuatavyo:

"Lalamiko na hati rasmi ya shtaka.

**104.-**(1) Mwenendo wa kesi unaweza kufunguliwa kwa kuwasilishwa lalamiko mbele ya mahakama na Mkurugenzi wa Mashtaka au Mwendesha Mashtaka Binafsi.

(2) Lalamiko litawasilishwa kwa njia ya maandishi na litasainiwa na Mwendesha Mashtaka wa Serikali au Mwendesha Mashtaka Binafsi aliyefungua mashtaka.

Utoaji wa hati ya wito.

**105.-**(1) Baada ya kupokea lalamiko kutoka kwa Mwendesha Mashtaka Binafsi, mahakama inaweza, kutoa hati ya wito au kibali kumtaka mshtakiwa kuhudhuria mbele ya mahakama yenye mamlaka ya kusikiliza kosa linalodaiwa kutendeka.

(2) Hati ya wito au kibali chochote kinaweza kutolewa na kutekelezwa baina ya saa 12:00 asubuhi hadi 12:00 jioni katika siku yoyote ya wiki ikijumuisha siku ya mapumziko, lakini mahakama inaweza kwa kibali, kumuidhinisha afisa polisi au mtu mwengine ambaye hati ya wito au kibali hicho kimepelekwa kwake kwa ajili ya kuitekeleza saa yoyote.

Kuondosha lalamiko.

**106.** Endapo, baada ya kuzingatia maelezo ya kiapo ya mlalamikaji au mashahidi wake, kama yapo, katika mashtaka binafsi na matokeo ya uchunguzi au upelelezi wa Mwendesha Mashtaka Binafsi, kama yapo, mahakama inaona kwamba hakuna sababu ya msingi kwa ajili ya kuendelea na kesi, italifuta lalamiko hilo na katika kila kesi kama hiyo, mahakama kwa ufupi itaeleza sababu zake za kufanya hivyo."

Marekebisho ya kifungu cha 151.

**11.** Kifungu cha 151 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuingiza maneno:

(a) "usafirishaji haramu wa binadamu, ugaidi, ufadhili wa ugaidi, ufadhili wa silaha za maangamizi baina ya maneno "kukwepa kodi" na "au" katika kifungu kidogo cha (1); na

(b) "kifungu cha 161 cha" baina ya neno "ya" na "Sheria" katika kifungu kidogo cha (6).

Marekebisho ya kifungu cha 152.

**12.** Kifungu cha 152 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta neno "alipokamatwa" liliyopo mwisho wa kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake maneno "alipofikishwa mahakamani".

Marekebisho ya kifungu cha 172.

**13.** Kifungu cha 172 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (1) kama ifuatavyo:

"(1) Endapo mshtakiwa ambaye anawakilishwa kwa mujibu wa sheria anakataa kosa, mahakama inaweza, baada ya kumshauri mwendesha mashtaka na wakili wa mshtakiwa, haraka iwezekanavyo, kufanya usikilizaji wa awali katika mahakama ya wazi mbele ya mshtakiwa na wakili wake na mwendesha mashtaka na mahakama itazingatia mambo ambayo hayabishaniwi baina ya wahusika wa kesi na ambayo yatasaidia uendeshaji wa kesi kwa njia ya haki na ya haraka."

Marekebisho ya kifungu cha 202.

**14.** Kifungu cha 202 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (4) mara baada ya kifungu kidogo cha (3) kama ifuatavyo:

"(4) Mrajis wa Mahakama Kuu, kabla ya mwezi wa Machi ya kila mwaka, na kwa kuzingatia kanuni na miongozo kama Jaji Mkuu atakavyoweza kueleza kila

baada ya muda, atatayarisha orodha ya watu wanaofaa na wenye sifa za kuwa wakalimani Zanzibar ambayo itatumika na mahakama tu."

Marekebisho ya kifungu cha 244.

**15.** Kifungu cha 244 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kufuta neno "wakati wa" baina ya maneno "yoyote" na "upelelezi" na kuweka badala yake maneno "baada ya kukamilika kwa".

Kuongeza kifungu kipya cha 244A.

**16.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 244A mara baada ya kifungu cha 244 kama ifuatavyo:

"Taratibu za mapatano ya kukubali kosa.

**244A**. Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 246 cha Sheria hii, endapo makubaliano ya mapatano ya kukubali kosa yamefanyika baada ya kukamilika kwa upelelezi au kabla ya kesi kufunguliwa yanayopelekea makubaliano ya kutomshtaki mshtakiwa, makubaliano hayo yatatekelezwa na wadaawa nje ya mahakama na kila mdaawa atastahiki nafuu zote zinazohusiana na mkataba batili au wenye kuweza kubatilika kuhusiana na makubaliano yaliyofanywa."

Marekebisho ya kifungu cha 247.

**17.** Kifungu cha 247 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuingiza maneno "Mahakama za Wilaya na" baina ya maneno "katika" na "Mahakama."

Marekebisho ya kifungu cha 299.

**18.** Kifungu cha 299 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza maneno "Isipokuwa kwa kiwango cha chini cha adhabu," mwanzo wa kifungu.

Marekebisho ya kifungu cha 309.

**19.** Kifungu cha 309 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa:

(a) kufuta maneno "chini ya Sheria ya Adhabu" baina ya maneno "kosa" na "kuamuru"; na

(b) kuingiza maneno "au kukusudia kutumia" baina ya maneno "kutumia" na "na ".

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAKAMPUNI, NAM. 15 YA 2013

Kusomwa.

**20.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Makampuni, Nam. 15 ya 2013 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekbisho ya kifungu cha 34.

**21**. Kifungu cha 34 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongeza kifungu kidogo kipya cha (5) mara baada ya kifungu kidogo cha (4) kama ifuatavyo:

"(5) Kampuni, ndani ya siku thelathini, itawasilisha kwa Mrajis notisi ya mabadiliko ya idadi ya wanachama kwa mujibu wa vifungu vidogo vya (2), (3) na (4) vya kifungu hiki."

(b) kuvipa nambari upya vifungu vidogo vya (5) na (6) kuwa vifungu vidogo vya (6) na (7).

Marekebisho ya kifungu cha 69.

**22.** Kifungu cha 69 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (4) kwa kufuta maneno "anayehusika na fedha" baina ya maneno "Waziri" na "anaweza".

Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 90.

**23.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 90 na kuweka badala yake kifungu kipya cha 90 kama ifuatavyo:

"Kutokutolewa kwa hati za hisa.

**90.-**(1) Kampuni au afisa mwengine yeyote wa kampuni hatotoa au hatohamisha hati ya hisa yoyote iliyopo.

(2) Kampuni, endapo kutakuwa na hati ya hisa iliyopo, itatoa tangazo katika Gazeti Rasmi na angalau katika magazeti mawili yenye mzunguko mkubwa, kwa mmiliki ikimtaka kukabidhi hati yake ya hisa, na ikiwa kampuni ya kigeni, tangazo litatolewa katika Gazeti Rasmi na angalau magazeti mawili yenye mzunguko mkubwa katika wilaya ambayo kampuni ilisajiliwa awali.

(3) Mmiliki yeyote wa hati za hisa zilizopo, ndani ya miezi sita kuanzia tarehe ya tangazo lililotolewa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, atakabidhi kwa kampuni hati za hisa alizopewa kwa ajili ya kufutwa, na mmiliki atasajiliwa kama mmiliki wa hisa hizo katika daftari la wanachama wa kampuni.

(4) Baada ya kukabidhiwa na kufutwa kwa hati za hisa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, kampuni na kila afisa wa kampuni atamjulisha Mrajis kuhusiana na mabadiliko hayo katika daftari la wanachama ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe ya kufutwa.

(5) Hati ya hisa yoyote ambayo haijakabidhiwa baada ya kumalizika kwa kipindi cha miezi sita itakuwa batili, na mmiliki hatakuwa na haki yoyote kuhusiana na hati hiyo.

(6) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, Mrajis anaweza kuwaruhusu wamiliki kukabidhi hati zao za hisa kwa kampuni baada ya kumalizika kwa kipindi cha miezi sita kwa kuwasilisha sababu za msingi zinazoeleza kuchelewa huko."

Kufuta na kuwekwa badala yake kifungu cha 91.

**24.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 91 na kuwekwa badala yake kifungu kipya cha 91 kama ifuatavyo:

"Adhabu kwa kujifanya mmiliki wa hisa.

**91.** Mtu yeyote ambaye kwa taarifa za uongo na udanganyifu anajifanya kuwa mmiliki wa hisa au ana maslahi yoyote katika kampuni, na kwa kufanya hivyo anapata au anafanya juhudi za kupata hisa au maslahi hayo,

au anapokea au anafanya juhudi za kupokea fedha zozote zinazodaiwa na mmiliki huyo kama ndiye mmiliki halali, ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atawajibika adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka saba."

Kufuta vifungu vya 92 na 118.

**25.** Vifungu vya 92 na 118 vya Sheria Mama vinafutwa.

Marekebisho ya kifungu cha 129.

**26.** Kifungu cha 129 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kuingiza neno "kalenda" baina ya maneno "kila" na "mwaka".

Kuongeza kifungu kipya cha 189A.

**27.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 189A mara baada ya kifungu cha 189 kama ifuatavyo:

"Marufuku kuteua mkurugenzi au mwanahisa mbadala.

**189A.** Kampuni haitoteua mkurugenzi mbadala au mwanahisa mbadala isipokuwa mkurugenzi mbadala wa kampuni binafsi yenye mwanahisa mmoja."

Marekebisho ya kifungu cha 195.

**28.** Kifungu cha 195 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta kifungu kidogo cha (2); na

(b) kuvipa nambari upya vifungu vidogo vya (3), (4) na (5) kuwa vifungu vidogo vya (2), (3) na (4) kwa mpangilio wake."

Kuongeza kifungu kipya cha 236A.

**29.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 236A mara baada ya kifungu cha 236 kama ifuatavyo:

"Uhifadhi wa kumbukumbu za kampuni baada ya kuvunjwa.

**236A.** Kampuni, wasimamizi, wafilisi au watu wengine wanaohusika katika kuvunjwa kwa kampuni watalazimika kuhifadhi nyaraka zote halisi zilizowasilishwa kwa Mrajis kwa kipindi cha miaka kumi kuanzia tarehe ambayo kampuni imevunjwa."

Kuongeza kifungu kipya cha 237A.

**30.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 237A mara baada ya kifungu cha 237 kama ifuatavyo:

"Uwezo wa Mrajis kufuta kampuni.

**237A.-**(1) Mrajis atatoa notisi ya maandishi kwa kampuni ya nia ya kuifuta kampuni hiyo katika daftari endapo atakuwa na sababu za msingi za kuamini kwamba:

(a) wakati wa kusajiliwa kwa kampuni, kulikuwa na upotoshaji au udanganyifu uliofanywa na kampuni;

(b) kampuni imejihusisha na vitendo vya uhalifu ikijumuisha utakatishaji fedha, usafirishaji haramu wa binadamu, usafirishaji haramu wa dawa za kulevya au ufadhili wa ugaidi; au

(c) kampuni inaendesha shughuli zake kinyume na malengo kama yalivyoainishwa katika katiba na kanuni za Kampuni.

(2) Kampuni inaweza, ndani ya siku thelathini baada ya kupokea notisi iliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kuwasilisha kwa maandishi kwa Mrajis sababu zinazoeleza kwa nini kampuni isifutwe katika daftari.

(3) Endapo kampuni itashindwa kutoa sababu ndani ya muda uliowekwa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki au endapo sababu zilizotolewa sio za kuridhisha, Mrajis ndani ya siku kumi na nne, ataifuta kampuni katika daftari na atatangaza katika Gazeti la Serikali jina la kampuni iliyofutwa, na kuijulisha kampuni juu ya uamuzi huo pamoja na sababu za uamuzi huo.

(4) Endapo kampuni, mwanachama au mdai hajaridhika na uamuzi chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, ndani ya miaka mitano kuanzia tarehe ya kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali, ataiomba mahakama kurejeshwa kwa kampuni katika daftari, isipokuwa kwamba, Mrajis, ndani ya kipindi cha miaka mitano, hatosajili kampuni nyengine kwa jina hilo.

(5) Mahakama inaweza, baada ya kupokea ombi la kurejeshwa kwa kampuni chini ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki:

(a) kuagiza kurejeshwa kwa kampuni katika daftari; na

(b) kutoa maelekezo na masharti kwa ajili ya kuiweka kampuni na watu wengine katika nafasi sawa kwa kadri itakavyowezekana kama kampuni haikufutwa.”

**31.** Jadweli la Kwanza la Sheria Mama linarekebishwa katika Sehemu ya Pili kwa kufuta kanuni ya 2(d). Marekebisho ya Jadweli la Kwanza.

**SEHEMU YA TANO**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR, NAM. 4 YA 2013**

**32.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Shirika la Utangazaji Zanzibar, Nam. 4 ya 2013 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama “Sheria Mama”. Kusomwa.

**33.** Kifungu cha 6 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza aya mpya ya (j) na (k) mara baada ya aya ya (i) kama ifuatavyo: Marekebisho ya kifungu cha 6.

“(j) kuingia, kujihusisha na kuendeleza biashara kama mtengenezaji na msambazaji wa maudhui ya televisheni na huduma zinazohusiana na mitandao ya kijamii; na

(k) kufanya kazi nyengine yoyote kwa ajili ya kufanya biashara ya uunganishaji na usambazaji wa maudhui".

Marekebisho ya kifungu cha 7.

**34.** Kifungu cha 7 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza aya mpya ya (f) na (g) mara baada ya aya ya (e) kama ifuatavyo:

"(f) kuanzisha na kuendesha huduma za masafa marefu katika utangazaji wa kidijitali, kuweka na kuandaa vituo vya utangazaji, studio, mifumo ya usafirishaji na miundombinu mengine kwa ajili ya kusambaza na kupokea programu za kidijitali kwa kutumia aina yoyote ya teknolojia ya habari na mawasiliano; na

(g) kuanzisha na kuendesha mfumo wa vituo vya mauzo unaoendana na uhalisia wa kibiashara ya uunganishaji na usambazaji wa maudhui kwa ajili ya kukuza biashara ya Shirika na kuimarisha utoaji wa huduma kwa wateja."

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR, NAM. 12 YA 2018

Kusomwa.

**35.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar, Nam. 12 ya 2018 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 35.

**36.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 35 na kuweka badala yake kifungu kipya cha 35 kama ifuatavyo:

"Wajibu wa taasisi za Serikali.

**35.** Taasisi zote za Serikali zitawajibika kupata huduma za uchapaji, vifaa vya kuandikia na vifaa vya ofisini kutoka kwa Wakala au taasisi nyengine ya Serikali iliyopewa uwezo na sheria."

## MADHUMUNI NA SABABU

Madhumuni ya Mswada huu ni kupendekeza marekebisho ya sheria mbalimbali ili kushughulikia changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa sheria hizo. Marekebisho hayo yanalenga kuondoa vikwazo vinavyoikabili Serikali katika maeneo mbalimbali na kuhakikisha sheria husika zinaendana na mahitaji ya sasa pamoja na mapendekezo ya Kikosi Kazi cha Kimataifa cha Kudhibiti Uhalifu wa Fedha yaliyotolewa baada ya ukaguzi uliofanywa katika maeneo yanayohusiana na sheria hizo.

Aidha, Mswada huu unapendekeza marekebisho katika Sheria ya Shirika la Utangazaji Zanzibar, Nam. 4 ya 2013, kufuatia uamuzi wa Serikali wa kuivunja Kampuni ya Usambazaji Maudhui Zanzibar (ZMUX) na kuhamisha majukumu yake kwenda kwa Shirika la Utangazaji Zanzibar, ili kuliwezesha Shirika hilo kutekeleza majukumu hayo kwa mujibu wa Sheria. Pia Mswada unapendekeza marekebisho ya Sheria ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar, Nam. 12 ya 2018 kwa kuweka utaratibu wa kisheria na kuipa taasisi nyengine uwezo wa kutoa huduma za uchapaji.

Mswada huu umegawanywa katika Sehemu Sita:

***Sehemu ya Kwanza:*** inahusu masharti ya awali yanayojumuisha jina fupi na kuanza kutumika kwa Sheria pamoja na marekebisho ya sheria mbalimbali.

***Sehemu ya Pili:*** inarekebisha kifungu cha 10 na 10C cha Sheria ya Udhibiti na Utakatishaji wa Fedha Haramu na Mapato yatokanayo na Uhalifu, Nam. 10 ya 2009 kwa lengo la kuimarisha mbinu ya tathmini ya viashiria hatarishi katika mapambano dhidi ya utakatishaji wa fedha na ufadhili wa ugaidi, kuimarisha hatua zinazohusiana na watu wenye wadhifa maalumu, na kuhakikisha upimaji wa kitaifa wa hatari unaofanyika mara kwa mara kulingana na viwango bora vya kimataifa. Mambo haya yote yanatokana na mapendekezo ya Kikosi Kazi cha Kimataifa cha Kudhibiti Uhalifu wa Fedha Haramu.

***Sehemu ya Tatu:*** inalenga kurekebisha vifungu mbalimbali vya Sheria ya Mwenendo wa Makosa Jinai, Nam. 7 ya 2018 ili kuimarisha taratibu za upelelezi na uendeshaji wa mashauri ya jinai, kufafanua maana ya maneno muhimu, kuimarisha haki zinazolenga mhanga wa kosa, kuanzisha mbinu za kisasa za uchunguzi kama vile usafirishaji uliodhibitiwa, mitego na operesheni za siri, kuweka taratibu za makubaliano ya kumaliza kosa, na kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa mashauri ya jinai na ushughulikiaji wa ushahidi.

***Sehemu ya Nne:*** inapendekeza marekebisho mbalimbali ya Sheria ya Makampuni, Nam. 15 ya 2013 kwa lengo la kuimarisha uwazi na uwajibikaji wa makampuni, kupiga marufuku utoaji na matumizi ya hati za hisa, kuzuia matumizi ya wanahisa na wakurugenzi mbadala, kuimarisha mamlaka ya Mrajis wa Kampuni ya kufuta usajili wa makampuni yanayojihusisha na shughuli haramu au za udanganyifu, kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu baada ya kuvunjwa kwa kampuni,

na kulinganisha usimamizi wa makampuni na mahitaji ya kuzuia utakatishaji wa fedha na maslahi ya umma.

***Sehemu ya Tano:*** inahusu marekebisho ya kifungu cha 6 na 7 cha Sheria ya Shirika la Utangazaji Zanzibar, Nam. 4 ya 2013. Madhumuni ya marekebisho hayo ni kulifanya Shirika kutekeleza kazi zilizokuwa zikifanywa na Kampuni ya Kusambaza Maudhui (ZMUX) kwa lengo la kutekeleza agizo la Serikali baada ya kuivunja Kampuni hiyo ya ZMUX. Pia, marekebisho hayo yataliwezesha kujiongezea mapato yatakayotokana na kazi hizo ili liweze kujimudu katika kujiendesha.

***Sehemu ya Sita:*** inahusu marekebisho ya kifungu cha 35 cha Sheria ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar, Nam. 12 ya 2018 kwa lengo la kutoa fursa kwa taasisi ya Serikali nyengine yenye uwezo wa kisheria wa kutoa huduma za uchapaji ili kuongeza ufainisi na upatikanaji wa huduma za uchapaji kwa taasisi za Serikali.



**ZANZIBAR**
**18 Agosti, 2026**

**(DKT. MWINYI T. HAJI**
**MWANASHERIA MKUU**
**ZANZIBAR**

LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR 2026